**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA RAIS- TAMISEMI.**

SHULE YA SEKONDARI ANNA MKAPA,
S. L. P 8824,
MOSHI.
TAREHE ……………………....

Namba za simu:
MKUU WA SHULE: 0688 460 242/ 0754 824 621
MAKAMU MKUU WA SHULE: 0784954828/ 0767954828
PATRON: 0688 406 655/ 0753 096 504

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ………………………………………..
…………………………………………………………………………………..
S. L. P ……………………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ANNA MKAPA, HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI. MKOA WA KILIMANJARO MWAKA ………………………….**

**1**. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka ………………….Tahasusi ya **PCB** Shule ya sekondari Anna Mkapa ipo umbali wa km 3 kutoka stendi kuu ya mabasi ya Moshi Mjini barabara ya kuelekea Pasua .Usafiri wa kutoka stendi ya mabasi Moshi Mjini unapatikana kwa kutumia mabasi ya kwenda Pasua utashuka kituo cha msikitini kwa nauli ya Tsh 400/=.Au stendi ya mabasi ya Moshi Mjini mabasi yatokayo KCMC kwenda Getifonga unashuka kilipo kibao cha shule kituo cha Temere kwa nauli ya shs. 400/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **……………………..** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…………………….** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **………………**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**2.1. SARE YA SHULE**

a) Sare ya shule ni suruali mbili (2) KAKI ziwe na makunjo mawili mbele kila upande na mfuko mmoja nyuma na kunjo la (turn up) chini na suruali zisiwe nyembamba ziwe na inchi kumi na nane (18) na mashati mawili meupe (2) mikono mifupi.(Aje nazo )
b) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2) vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi..
c) Soksi nyeusi jozi nne.
d) Bukta na fulana ya dark blue na raba kwa ajili ya michezo.

e) Sweta ya rangi ya suruali yenye shingo V.
f) Nguo za kushindia suruali mbili nyeusi mshono sawa na sare ya shule na fulana (Tshirts) mbili zenye kola na zinapatikana shuleni kwa bei ya shs. 10,000/= @ taslimu.
g) Mkanda wa kuvalia suruali wa ngozi mweusi.
h) Nguo za kulalia pajama zisizopungua jozi mbili na sweta/ jacket kwa ajili ya baridi jioni.

**2.2**:**ADA NA MICHANGO YA SHULE**

a). Ada ya shule kwa mwaka itakuwa shilingi elfu sabini (70,000) kwa mwanafunzi wa bweni .Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili ambayo ni kiasi cha elfu thelathini na tano (35,000) kwa muhula.

b). **Michango inayotakiwa kulipwa na kila Mzazi ni:**
i) Sh. 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii) Sh. 5,000/= kwa ajili ya tahadhari (haitarejeshwa)
iii) Sh. 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
iv) Sh. 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa walinzi, wapishi na vibarua wengine.
v) Sh. 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
vi) Sh. 3,000/= kwa ajili ya nembo ya shule.
vii) Sh.15,000/= kwa ajili ya matibabu 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na 5,000/= kwa ajili ya bima ya afya kama mwanafunzi ana bima atatoa sh. 10,000/= ya huduma ya kwanza.
viii) Sh. 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima mock (kidato cha sita)
ix) Mwanafunzi anayelipiwa na Halmashauri au Taasisi yoyote aje na utambulisho wa barua.
**NB: Fedha zote zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. 40301200141 MMC ANNA MKAPA SECONDARY katika benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip halisi na aje nayo) Fedha taslimu hazitapokelewa.**

**C: Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anatakiwa kuleta shuleni ni;**
i) Ream moja ya karatasi A4 (photocopy paper) kwa mwaka
ii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia.
iii) Scientific calculator na Digital stop watch
iv) Godoro la sponji (Inch. 3)
v) Mashuka jozi 2 rangi ya blue, blanket moja, mto mmoja, foronya mbili rangi ya shuka na chandarua kimoja pembe nne ndogo.
vi) Vyombo vya kulia chakula (sahani, kikombe, bakuli na kijiko)
vii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
viii) Taulo, miswaki, dawa ya meno, ndala, sabuni ya kufulia na kuogea za kutosha.
ix) Tochi ya kuchaji kwa mwanga wa jua/betri, mishumaa hairuhusiwi.
x) Mabuti, mwavuli au koti la mvua
xi) Lab coat nyeupe.
xii) Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa na matokeo ya kidato cha nne (Result slip)
xiii) Unatakiwa uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi:
- Dekio aina ya pusher (dryier) ya kusukuma maji / hard broom(brush ngumu)
- Ufagio mrefu wa chelewa
- Jembe 1 lenye mpini /rake

**3.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**
**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE.**

1. Wizi.
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro.
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi wenzake, walimu, /walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote.
6. Kufuga ndevu
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya mfano kuberi, cocaine .
9. Uvutaji wa sigara.
10. Kushiriki matendo ya uhalifu , siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi .
11. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
12. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
13. Kumiliki au kukutwa na simu ya mkononi au line ya simu katika mazingira ya shule au kutumia simu za wafanyakazi, walimu au mtu yeyote.

14 Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
15. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
16. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. VIFAA VYA MAFUNZO.**
**A. VITABU.**
Shule haina vitabu Wazazi wawanunulie watoto wao vitabu vya masomo husika.
Mzazi/ Mlezi anatakiwa amnunulie mwanae vitabu vifuatavyo:

**PHYSICS**
i)Advanced level physics Author Nelkon and Parker
ii)Advanced level physics material and Mechanics Duncan 1and 111
iii)Fundamental Exercise in physics Author G.R.A Tit Comb Revised & Jackson
iv)Progressive Exercise in physics author C. Wilson
v) Principle of physics by Chands
vi) Calculations for A- level physics by T. L.Lowe & J.F Rounce
vii) Schaum's solved problems series 3000 solved problems in physics, publisher Tata Mc Graw Hillpub Ltd New-Delhi-India . Author Alvin Halpern Ph.D.
viii) Principle of physics by Chands

**CHEMISTRY**
i) Advanced level chemistry by E. N. Ramsden
ii) Organic chemistry by Robert t. Morrison &R. N.Boyd
iii) General chemistry by Holtzelaw Robson
iv) Calculations for A-level by E.N.Ramsden
v) Calculations for A-level chemistry fourth Edition by E.N. Ramsden
vi) Conceptual chemistry for class XI publisher Schand co. Ltd by S. K.Iain

**MATHEMATICS**
(i)Advanced mathematics by Kinunda

(ii)A Level mathematics by L .Shayo
(iii)Advanced mathematics by Tranter
(iv)Advanced statistics by Schaum's series
(v)Logic and set by Schaum's
(vi)Advanced maths rev .questions and answers 1999-2006 UDSM by Hermes
(vii) Pure mathematics 1&2 by J.K Backhouse

GENERAL STUDIES

(i)Advanced general studies by Dr. Nyirenda
(ii)Advanced level general studies notes (Necta syllabus approach for form v & vi ) by G. Mshiu
(iii)Advanced level general studies questions and answers form v and vi by Masuko Christopher Saluhaya.
(iv) African Bible published by Paulies Publications Africa or Aplication Study Bible

BIOLOGY.

(i) Biology science by Taylor Green Stout
(ii) Understanding Biology

**B**. **VIFAA VINGINE VYA MASOMO**.

1. Daftari kubwa yasipungue **7**
2. Mathematical set, kalamu za wino, risasi, rula n.k.
3. Vitabu vya ibada kwa mujibu wa madhehebu / dini yako.

**5. FEDHA ZA MATUMIZI MADOGO MADOGO (POCKET MONEY).**

Mzazi anaweza kumpa mwanafunzi kiasi cha fedha cha kuridhisha lakini zitunzwe benki ili kuondoa vishawishi vya wizi.

**6. MAMBO MENGINE MUHIMU**.

i) **FOMU ZILIZOAMBATANISHWA**.

A. Hati ya makubaliano
B. Fomu ya uraia
C.Fomu ya Uchunguzi wa afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali . Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara atakaporipoti shuleni.
D. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
E. Fomu ya usajili wa mwanafunzi.
F. Fomu ya ahadi na picha za wazazi /walezi na ndugu wawili.

**MUHIMU:** Tafadhali soma kwa makini maelezo, maelekezo na maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA ANNA MKAPA SEKONDARI.**

…………………………………

**MKUU WA SHULE**
**ANNA MKAPA SEKONDARI.**

**FOMU A**
**HATI YA MAKUBALIANO.**

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI ANNA MKAPA,
S. L. P 8824,
MOSHI.

**YAH: KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE.**

Mimi ………………………………………………….. Nakubali nafasi ya kidato cha …………………..Niliyopewa katika shule yako.
Ninayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule hizo zilizoko na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu. Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii walimu wote wa shule na wafanyakazi kama walezi wangu.

Naahidi kuwa nitatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa viongozi kwa mujibu wa sheria.
Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu na naahidi pia kuwa nitajielimisha kwa nguvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu kwa ujumla. Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza nafasi yangu hapa shuleni.

JINA …………………………………………….. SAHIHI …………………
MWANAFUNZI MWANAFUNZI

JINA LA MZAZI /MLEZI …………………………………………………..
SAHIHI ……………………………………………………………………
MZAZI / MLEZI /MWANAFUNZI

ANWANI YA MZAZI / MLEZI…………………………………………….
SIMU…………………………………………………………………...
Email…………………………………………………………………….

Namba ya kuandikishwa (Admission No.) ……………………..Tarehe ……………
Darasa ulilopangiwa ……………………………..Bweni …………………………….
Jina la mwalimu wa malezi ………………………………..Sahihi……………………

**FOMU B**

ANNA MKAPA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 8824,
MOSHI.

MEDICAL OFFICER,
…………………………………………………………
…………………………………………………………
…………………………………………………………

To be completed by medical officer from a recognized **Government Hospital**,
Name of student ………………………………………………………………………..

Blood count (Red and White) ………………………………………………………….
Stool examinations ……………………………………………………………………..
Sexually Transmitted Diseases ………………………………………………………...
T.B ………………………………….Skin …………………………………………….
Eye test ………………………………Ears ……………………………………………
Chest …………………………………Spleen …………………………………………
Abdomen ……………………………………………………………………………….

**ADDITIONAL INFORMATION**.

Physical defects /impairment pediatric disorders ………………………………….
I certify that the above is fit /unfit to pursue studies as stated above.

Signature ………………………………………………………………………………
**MEDICAL OFFICER**

DATE ……………………………………………….Rubber Stamp

NOTE: Student should send or bring the completed form to school together.

**FOMU C**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**

SHULE YA SEKONDARI ANNA MKAPA, S. L. P 8824, MOSHI.

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**.

1. Andika majina kamili

i)Majina ya shule …………………………………………………………………

ii)Majina ya nyumbani ……………………………………………………………

| | JINA | BABA | UKOO | UMRI | TAREHE YA KUZALIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| LAKO | | | | | |
| LA BABA | | | | | |
| LA MAMA | | | | | |

2.NYUMBANI.

Kijiji/ Mtaa ………………………………….Kata ……………………………………
Tarafa ……………………………………Wilaya …………………………………..

3. Anwani ya nyumbani ……………………………simu ……………………………
4. Kukiwa na matatizo taarifa ipelekwe kwa nani (jina) ………………………………
Simu ……………………………………….
Uhusiano na wewe ……………………………………………………………….
Anafanya kazi gani na wapi ………………………………………………………

5. Wazazi na ndugu:
Baba yuko hai? ………………………. Mama yuko hai? …………………………….
Baba ana watoto wangapi ……………wavulana…………wasichana…………….
Wewe ni mtoto wa ngapi ? …………..Baba ana wake wangapi? ……………………..
Wewe ni mtoto wa mke wa ngapi? ……………….Mko wangapi kwa mama huyo?
………………Wewe ni wa ngapi kwa mama huyo? ………………………………
6. Dini yako …………………………Madhehebu …………………………………

**UNAOWATEGEMEA**.

7.Unaishi na nani na wapi? ……………… Simu yake ……………………………...
Nani anayekupa mahitaji ya shule ……………………Simu yake ………………….
Toa sababu kama siyo Mzazi ……………………………………………………..

**FOMU D**

FOMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI, WAZAZI/ WALEZI WAWILI NA NDUGU WAWILI PICHA ZAO ZIAMBATANISHWE KWENYE VISANDUKU.

**AHADI YA MWANAFUNZI.**

Mwanafunzi ……………………………………………………………………………
Ninaahidi kufuata taratibu na sheria zote za shule ikiwa ni pamoja na kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

SAHIHI ………………………………  TAREHE ………………………………

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**.

Mimi Mzazi wa Mwanafunzi ………………………………………………………..
Kidato cha ………………………………….Mwaka ……………………………….
Ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango ya shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule kwa kipindi chote mwanangu atakapokuwa katika Shule ya Sekondari Anna Mkapa.

JINA LA MZAZI/ MLEZI.
1 ……………………………..  2 ………………………………

SAHIHI ……………………………….. SAHIHI …………………………………

TAREHE ……………………………… TAREHE ………………………………..
NDUGU WAWILI
3. JINA……………………………….4.JINA……………………………………

SAHIHI……………………………..  SAHIHI ……………………………….